



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 14/07/2023

TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA KWA AJILI YA UJENZI WA UJENZI WA
MADARASA NA MATUNDU YA VYOO KATIKA SHULE ZA MSINGI

ZABUNI NA: LGA/071/2022/2023/RDC/W/6 LOT 1- 4

1. **Mkurugenzi Mtendaji (W)** anawatangazia Wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa **Chumba kimoja (1) cha Darasa na Matundu Sita (6) ya Vyoo** katika **Shule za Msingi za Katumba I, Bulyaga, Iponjola na Mabonde** kupitia **Programu ya Mradi wa SEQUIP** kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
2. Ujenzi wa **Miundo mbinu ya Shule** inatarajiwa kujengwa katika shule za Msingi kwa mchanganuo ufuatao:-

Zabuni Na.	KITALU (LOT) NA.	JINA LA SHULE YA MSINGI	MIUNDO MBINU
LGA/071/2023/2024/RDC/W/6	1	Katumba I	Ujenzi wa Darasa 1 na matundu 6 ya vyoo
	2	Iponjola	Ujenzi wa Darasa 1 na matundu 6 ya vyoo
	3	Bulyaga	Ujenzi wa Darasa 1 na matundu 6 ya vyoo
	4	Mabonde	Ujenzi wa Darasa 1 na matundu 6 ya vyoo

3. Hivyo basi, **Mkurugenzi Mtendaji (W)** anakaribisha Mafundi ujenzi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za ujenzi wa **Miundo mbinu ya Serikali** kuomba kazi za **Ufundi** kwa utaratibu wa **"Force Account"** katika fani na sifa za **Ufundi** zifuatazo:-

i. **Fundi Uashi (Ujenzi wa Msingi, Kuta na Rinta),**

- Awe na elimu ya ufundi Uashi/ujenzi na mwenye kujua kusoma ramani za majengo.
- Awe na vitendea kazi za kunyoosha ukuta kama vile Square, bridge (Plumb Bob), mwiko, Komabao, Pima maji n.k

- ii. **Fundi Lipu na Koplo (inahusisha unyoshaji wa kuta)**
 - Awe na ujuzi na uzoefu katika upigaji plaster na koplo kwenye majengo ya Serikali ulio nadhifu.
 - Awe na vitendea kazi za kunyoosha ukuta kama vile Rati, Pima maji, Mwiko, Mkono bao n.k

- iii. **Fundi Aluminium**
 - Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani.
 - Awe na uwezo wa kutengeneza madirisha ya Aluminium na milango ya alco bond).
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

- iv. **Fundi Seremala (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).**
 - Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya mbao ngumu
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

- v. **Fundi kupaua, brundering, kufunga Gypsum na gutter**
 - Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani
 - Awe na uwezo wa kupaua majengo ya Serikali kwa kutumia mbao laini.
 - Awe na uwezo wa kupiga dari (brundering) na kufunga Gypsum
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

- vi. **Fundi bomba (inahusisha ufungaji wa mifumo ya maji safi na maji taka)**
 - Awe na ujuzi wa Ufundi Bomba kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali.
 - Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani

- vii. **Fundi Rangi (inahusisha skimming, chupping na upakaji wa rangi)**
 - Awe na ujuzi na uzoefu wa kupaka rangi majengo ya umma na binafsi
 - Awe na uwezo wa kuchanganya rangi mbalimbali za majengo

- viii. **Fundi umeme (inahusisha ufungaji wa conduit kwenye ukuta na wiring)**
 - Awe na ujuzi wa Ufundi Umeme kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali.
 - Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani

- Awe na uwezo wa kusuka na kufunga mifumo ya umeme
- Awe na uzoefu wa kusuka umeme kwenye majengo ya Serikali

4. Pamoja na sifa zilizotolewa hapo juu waombaji wanapaswa kuzingatia masharti kama ifuatavyo:-

- Awe Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
- Awe na Namba ya Utambulisho wa mlipa kodi (TIN) (aambatanishe na barua ya maombi kwa uthibitisho zaidi)
- Awe na akaunti ya benki kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe.
- Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Mtaa anakoishi.
- Awe tayari kufanya kazi muda wote hadi mradi utakapokamilika

5. Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu ziwasilishwe ofisi za Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi, S.L.P 148, Tukuyu yakiwa yamefungwa kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi ya Ufundi unaoombwa mfano **Ufundi Uashi au Seremala n.k**

6. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi za ufundi ni siku ya Ijumaa ya Tarehe 21/07/2023 kabla ya saa 4:00 Asubuhi. Aidha, maombi yatakayoletwa baada ya hapo hayatakubaliwa.

7. Waombaji wote wanatakiwa kuhudhuria usaili wa mafundi wa utakaofanyika tarehe 21/07/2023 saa 4:30 Asubuhi utakaombatana na kuwashindanisha nukuu za bei za ufundi.

8. Wako katika ujenzi wa Taifa



Mchali, R.B

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE